

جمعية الدعوة والإرشاد وتوعية الجاليات بالزلفي مبتروع تَعَلَّم الإسلام – أحكام الصلاة - سواحيلي

Samo la 9

الدرس التاسع

SUNNAH ZINAZO AMBATANA NA SWALA ZA FARADHI. (RAWATIBU).

Inapendekezwa kwa kila muislamu wa kike na wakiume, azihifadhi na kudumu nazo rakaa kumi na mbili za sunnah akiwa sio msafiri.

Rakaa mbili hizo ni rakaa nne kabla ya adhuhuri, rakaa mbili baada ya adhuhuri, rakaa mbili baada ya magharibi, rakaa mbili baada ya Ishai na rakaa mbili kabla ya swala ya alfajir.

فعن أم حبيبة - رضي الله عنها - قالت: سمعت رسول الله ﷺ يقول: ((مَا مِنْ عَبْدٍ مُسْلِمٍ يُصَلِّيَ لِلَّهِ كُلَّ يَوْمٍ ثِنْتَيْ عَشْرَةَ رَكْعَةً تَطَوُّعًا غَيْرَ فَرِيضَةٍ إِلَّا بَنَى اللَّهُ لَهُ بَيْتًا فِي الْجَنَّةِ ، أَوْ إِلَّا بُنِيَ لَهُ بَيْتٌ فِي الْجَنَّةِ)) [رواه مسلم: 728].

(Hakuna mja yeyote muislamu mwenye kuswali kila siku rakaa kumi na mbili za sunnah, isipokuwa Allah atamjengea nyumba peponi, au atajengewa nyumba peponi) (Ameipokea Imamu Muslim : 728).

Ni vyema kuswali hizi sunnah za rawatibu zinazo ambatana na swala za faradhi kuswaliwa msikitini, ama sunnah nyinginezo ni vizuri ziswaliwa nyumbani.

قال ﷺ: ((إذا قضى أحدكم الصلاة في مسجده، فليجعل لبيته نصيباً من صلاته، فإن الله جاعلٌ في بيته من صلاته خيراً)) (رواه مسلم: 778)
(Atakapo maliza mmoja wenu swala yake msikitini, basi ajaalie nyumbani kwake sehemu ya swala yake, kwa hakika ya mwenyezi mungu anaweka kheri ya haraka kwenye nyumba yake kutokana na swala yake ya sunnah aliyoisali nyumbani.) (Ameipokea Imamu Muslim : 778).

عن زيد بن ثابت - رضي الله عنه - قوله ﷺ: ((... فَإِنَّ خَيْرَ صَلَاةِ الْمَرْءِ فِي بَيْتِهِ، إِلَّا الصَّلَاةَ الْمَكْتُوبَةَ)) [متفق عليه: 6113، 781].
(Hakika ya swala bora anayoiswala mtu, ni lie swala anayoiswali nyumbani kwake isipokuwa swala ya faradhi) (Ameipokea Bukhar na Muslim : 6113, 781).

SWALA YA WITRI.

Inasuniwa kwa muislamu kuitekeleza swala ya witri, nayo ni sunnah iliyosisitizwa sana, na wakati wake wa kuiswali ni kuanzia baada ya swala ya Ishai mpaka kuchomoza Alfajir, na wakati wake mzuri kuiswali ni mwisho wa usiku kwa yule mwenye yakini ya kuamka usiku huo, swala hii ni miongoni mwa sunnah ambazo Mtume (saw) hakuiacha bali alikuwa akidumu nayo kwenye safari na hata akiwa hasafiri, na uchache wa rakaa zake ni rakaa moja.

Na alikuwa Mtume wa Allah akiswali usiku rakaa kumi na moja, kama ilivyopokewa Hadithi ya mama Aisha (R.A) :

((كان رسول الله ﷺ - يصلي بالليل إحدى عشرة ركعة، يوتر منها بواحدة... الحديث)) [رواه مسلم: 736]
(Hakika mtume wa Allah alikuwa akiswali swala za usiku rakaa kumi na moja, na akiswali witri rakaa moja) (Ameipokea Imamu Muslim: 736).

Swala za usiku ni rakaa mbili mbili kama ilivyokuja kwenye hadithi ya Ibn Umar (R.A) kwamba kuna bwana mmoja alikuja kwa mtume (saw) akimuuliza kuhusu swala za usiku Mtume akamjibu swala za usiku za sunnah ni rakaa mbili mbili :

عن ابن عمر رضي الله عنهما، أن رجلاً سأل رسول الله ﷺ - عن صلاة الليل، فقال رسول الله ﷺ: ((. صلاة الليل مثنى مثنى، فإذا خشي أحدكم الصبح، صلى ركعة واحدة، توتر له ما قد صلى)) [رواه مسلم: 749].

(Mtume amesema : (Swala ya usiku ni rakaa mbili mbili, basi akiechelea mmoja wetu kuwa asubuhi itampita, ataswali rakaa moja, na ataandikiwa kuwa ameswali swala ya witri) (Ameipokea Imamu Muslim : 849).

Inapendekezwa mara nyingine akunuti baada ya kurukuu katika swala ya witri, kwa Hadithi ya Hassan bin Aliy (R.A) pale ambapo Mtume (saw) alimfundisha maneno ayaseme katika dua ya swala ya Witri, lakini asidumu nayo.

Kwa hakika wengi wa wanavyuoni walioelezea swala ya Mtume (saw) hawakutaja kunuti yake Mtume (saw).

Kama inavyopendekezwa kwa yule ambae imempita swala ya usiku anaweza kuikidhi mchana kwa kuswali rakaa mbili, rakaa nne, rakaa sita, rakaa nane, rakaa kumi au rakaa kumi na mbili kwa kufuata alivyofanya mtume (saw).